GLOBAL ALLIANCE FOR GREEN AND GENDER ACTION



# Kujenga ustahmilivu/ udhibiti katika wakati ambao haijawahi kutokea

Mnamo mwaka 2020, Wanawake kote ulimwenguni walikuja pamoja na kuimarisha mifumo ya jamii katika udhibiti wa ustahamilivu, Ili kudumisha na kuimarisha maisha ya jamii zao na sayari katika kupambana na kukabiliana na changamoto kubwa zinazowakabili. Kwa GAGGA na vikundi vya washirika wetu, janga la COVID-19 liliwasilisha hali isiyo na kifani ambayo ililazimu ukaguzi na marekebisho ya mambo tuliyoyapa kipaumbele na Ratiba kwa jumla. Ambapo ilipoelekea washirika wa GAGGA kupitia vizuizi vingi hadi ikawaliazimu kutengeza njia mpya ya mawasiliano, kujenga uhusiano na mashikamano, na kuendeleza mipangilio.




Picha: RENAMAT

**Takwimu ya GAGGA: mwaka wa 2020**

**426** Mashirika ya kijamii yapatao ya wanawake yaliungwa mkono na kuwezeshwa na GAGGA.

**79%** Asilimia sabini na tisa yalifanikiwa kupokea jumla ya Euro milioni mbili nukta mbili €2.2M katika ruzuku.

**21%** Asilimia ishirini na moja ilipokea ufadhili usio wa kifedha pekee.

## Mpangilio katika nafasi za kidigitali

Washirika wa GAGGA Walisaidia Pakubwa katika kuhakikisha **matumizi salama na yenye ufanisi ya zana za kidijitali na kushiriki kwa vikundi vya wanawake vilioko chini mashinani.** Mikakati iliyojumuishwa katika utekelezaji huo ni pamoja na: ununuzi wa vifurushi vya data kwa simu za rununu; Kutoa na kuhakikisha usafiri salama kwa maji au kijiji kilichoko karibu pamoja na kuhakikisha uwepo na upatikanaji wa mitandao; kuimarisha ujuzi wa matumizi ya tarakilishi; na kupeana mafunzo ya namna au jinsi ya kushiriki katika anga za mitandaoni kitaifa na kimataifa.

**International Analog Forestry Network** (Mtandao wa analogi kimataifa wa misitu) ulianzisha nafasi ya kidijitali kwa wanawake wakuzaji wa misitu ya Analogi nchini Bolivia, Costa Rica, Nicaragua na EL Salvador. Kupitia ujumbe wa sauti na video, zilizopeperushwa kupitia programu za kutuma ujumbe kama vile WhatsApp na Signal, walipeperusha kiutaalamu ufahamu kuhusiana na misitu ya analogi, Muundo na utekelezaji kwa kuwainua na kuwapanua wanawake, katika ufahamu pamoja na mbinu za kusaidia kuwafikia jamii zilizoko mashinani, hususan vijiji ambavyo havijaendelea wakilenga haswa wanawake . Nafasi hii ya kidigitali ilizua mazunguko wa kuwaminiana na kusaidiana miongoni mwa wanawake waendelezaji. **FRIDA, Mfuko wa vijana wa kike ilitoa** mfululizo wa maudhui kuhusu utunzaji na usalama wa kidijitali. Unaohusisha mada kama vile miundo mbinu msingi ya mtandao, programu za kutuma ujumbe salama, na utunzaji wa kidijitali unapotumia vifaa husika, vile vile tahadhari maalumu iliweza kutolewa kwa vijana wanawake wanaojihusisha na utetezi wa hali ya hewa na mazingira.

GAGGA, ilipanga mfumo pepe za pamoja kujenga maarifa na ufahamu wa kukumbuka, ambazo zilchangia pakubwa katika mchakato wetu wa nje kutathmini na kutoa mawazo kwa siku zijiazo. Mazungumzo haya yalisaidia kuelekeza maendeleo ya programu ya GAGGA ya **'Women Leading Climate Action' programme** (tazama hapo chini) na Jarida liliolenga viongozi wa wanawake katika utetezi wa haki za anga na mazingira . Wakishikiana na shirika la mazingira la wanawake na shirika la maendeleo pamoja na marafiki wa shirika la kimataifa la dunia, GAGGA iliandaa kikao katika mkutano wa kimataifa 'kutoka ground up' ulioandaliwa na muungano wa COP26. Kikao hicho, **Feminist Climate Action: (Kujenga uwezo katika kila daraja)** kilihudhuriwa na zaidi ya watu 150.

Ilizunduliwa mwaka wa 2016, shirika lisilokuwa la serikali Global Alliance for Green and Gender Action (muungamo wa kimataifa wa kijani na jinsia GAGGA) Inakusanya na kuleta pamoja nguvu za haki ya wanawake, harakati za haki za mazingira na hali ya hewa /anga ulimwenguni. Maono ya GAGGA Duniani ni kuhakikisha haki za wanawake katika kupata maji, Usalama wa chakula, Mazingira safi na yenye afya na salama zinatambuliwa na kuheshimiwa. Wanafadhiliwa na kuwezeshwa na Fondo Centroamericano de Mujeres (FCAM), Kwa ushirikiano na Mama Cash na Both ENDS. Kwa Maelezo na ufahamu Zaidi, Tembelea tovuti yetu, ama utufuate kwenye twitter pia unaeza kujiandikisha kwa jarida letu.

## Kukuza heshima ya haki za wanawake katika ngazi za vijiji na kitaifa

Washirika wa GAGGA waliendelea kuimarisha, mazoea yao endelevu, yanayohusiana na kuzingatia jamii, sio tu kuhakikisha mfumo wa maisha yao, bali pia usalama wa chakula upatikanaji wa maji safi na salama, bali pia kama njia ya kudumisha udhibiti ama kudai kurudishiwa kwa ardhi na mipaka yao. Juhudi hizi za ushawishi na utetezi wa vikundi vilivyoko mashinani vinavuo ungwa mikono na shirika la GAGGA vinazingiatia zaidi masuala kama vile kuregesha kitu kwa hali ya kawaida/ulinzi wa ekolojia (pamoja na bayoanuwai); kilimo endelevu; Mabadiliko ya tabia nchi; uwezesheji na uhuru wa kiuchumi miongomi mwa masuala mengine.

Nchini Indonesia, mipango ya maendeleo ya mradi wa nishati ya mvuke, umeme wa kutumia maji, na mashamba ya unyunyizaji kutumia upepo haijawahi kufanya mashauriano muafaka na wanajami ambao wangeathirika. Katika mwaka 2020 mshirika wa GAGGA **Aksi!** ilifanya **utafiti wa ushirikishi wa wanawake,** na kukusanya ushahidi kutoka kwa zaidi ya wanawake 50 kuhusiana na jinsi **walivyoathiriwa vibaya na miradi ya msharti mbadala.** utafiti huo ulikuwa msingi wa ripoti iliowasilishwa na Aksi!, pamoja na Save Gunung Slamet, kwa kamati ya CEDAW, ambayo ilisababisha ufuatiliaji kwa moja kwa moja na serikali ya Indonosia. Na majadiliano ya mezani na mtandao, 'wanawake katika maeneo husika ya miradi wanishati wazungumza', Aksi! iliangazia **masuluhisho yanayozingatia watu na njia mbadala** ambazo zimeendelezwa kidemocrasia na kukuzwa kiushirikishwaji, kwa kuzingatia mchango, ridhaa na udhibiti wa wanawake pamoja na jamii zinazopatikana mashinani.

**Kebetkache Women Development and Resource Centre** (maendeleo ya wanawake wa Kabetkache na kituo cha rasilimali) **Pamoja na Lokiaka Community Development Centre** (kituo cha maendeleo ya jamii cha Lokiaka), chenye makao yake huko Port Harcout, Nigeria, Walipeana ufahamu kuhusu mambo yanayo wakabili wanawake na jumuiya za wenyeji wanapopatikana Niger Delta kuhusiana na uchimbaji wa mafuta na uchomaji gesi (wakati makampuni ya mafuta yanayochoma gesi ambayo hutoka kwa sababu ya kuchimba mafuta aina ya oil). Ruzuku ya kuunganisha na mafunzo ya GAGGA ya mwaka wa 2019 ilisaidia kuimarisha kwa kukamilika kwa kazi za mashirika mawili, mnamo mwaka 2020, Kebetkache iliimarisha ufahamu wa wanawake katika jumuiya za Lolouma na Omuechem kuhusu **haki yao ya kusema 'hapana' kwa uwakaji wa gesi,** vilevile kuinua viwango vya ufahamu wao katika kutambua na kufafanua na kushirikiana pamoja na watoa maamuzi. Pia Kongomano lililohusisha wanajamii, mashirika yaliyosajiliwa kisheria ya jamii, na wakali si wa wizara za nje pamoja na wizara ya mazingira na wakala wa mwelekeo wa kakitaifa iliandaliwa, katika kongomano hilo, wizara ya masuala ya wanawake ya jimbo la Rivers ilijitolea kulipa kipaumbele zaidi masuala yaliojitokeza, hasa madhara kwa wanawake ya kuwaka kwa gesi na uchafuzi wa mazingira.

## Kudumisha Shinikizo kwa Taasisi za fedha za kimataifa

Licha ya vizuizi vilivyosababishwa na janga la COVID-19, GAGGA iliendelea kujihusisha, kushawishi na kuchangia katika ukuzaji wa maendeleo, uimarishaji na ufuatiliaji wa sera za kijamii na mazingira za taasisi za fedha za kimataifa. Kwa pamoja washirika na wanachama GAGGA wanaoshirikiana na Africa Development Bank (Benki ya maendeleo ya Africa), Asian Development Bank (Benki ya maendeleo ya Asia), Asian Infrastructure Investment Bank (Benki ya uwekezaji wa miundombinu ya Asia), Benki ya ulaya ya ujenzi na maendeleo na Benki ya maendeleo ya interamerican, walizingatia mahitaji ya dharura ya **tathmini ya mapendekezo ya mradi, vile vile na utelekezaji wa mradi ili kuzingatia sera za kijamii na mazingira za Benki.**

**Interamerican Association for environmental defense** (jumuiya ya kimataifa ya ulinzi wa mazingira, AIDA) iliendelea kujenga shinikizo kwa **Interamerican Development Bank** (Benki ya Maendeleo ya Interamerican, IDB) kuchukua hatua kuhusiana na miradi miwili mikubwa ya maji, Pojom II na San Andre's in Guatemala, ambayo inakiuka sera ya oparesheni ya Benki ya Usawa wa Jinsia, kati ya sera nyinginezo. Ingawa AIDA haikuweza kushiriki moja kwa moja na kushiriki katika nafasi rasmi zinazohusiana na IDB kutokana na janga hilo. Kikundi kiliendelea kuongeza ufahamu, kukemea hali hyo, na bora Zaidi, kuhakikisha kuendelea kuwasiliana na kuhimiza mshikamano na **Wanawake wa ndani wa Ixquisis** na jamii zao, ambao haki zao zimekiukwa na mradi. AIDA iliandaa nafasi kadha tofauti za mtandaoni na kampeni ya dua na mawasiliano mtandaoni, na kuongeza uelewa katika eneo lote kuhusu matokeo ya miradi na kujengwa usaidizi kwa jamii za Ixquisis.



Picha WoMin African Alliance

## Ushirikiano na mfuko wa Ufadhili wa hali ya hewa ya kijamii

Washirika wa GAGGA waliendelea kuendesha masomo na mafunzo ya kuwajengea uwezo ili kuongeza uelewa na kuhamisha vikundi vya kijamii vilivyoko mashinani kushiriki katika michakato ya **maamuzi ya mfuko wa ufadhili wa taifa wa hali ya hewa ya kijani (GCF).** GAGGA ilisaidia mashirika ya haki za wanawake nchni Indonesia, Mongolia, Nepal na Tanzania kuingia katika **mijadala ya kisera na mamlaka ya kitaifa iliyoteuliwa ya GCF** (NDA); kuongeza ushirikiano wao katika michakato ya kitaifa ya kufanya na kutoa maamuzi, kama vile kutoa utaalamu wa kijinsia kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na kutumia njia rasmi kushirikiana na serikali/NDA; na ufuatiliaji wa miradi inayoendelea sasa au iliyopangwa ya GCF katika nchi yao.

GAGGA, pamoja na wahusika wengine, pia waliendelea kuzingatia matakwa na mahitaji ya washirika katika michakato ya kimataifa ya kufanya maamuzi ya GCF, pamoja na kukuza ufikiaji wa ndani, mwitikio wa kijinsia na kufanya maamuzi ya pamoja. Wakati wa mikutano ya wanabodi ya mwaka wa elfu mbili na ishirini (2020), tulishauri **kuiboresha mipango ya kijinsia na tathmini ya jinsia** ya mapendekezo mbalimbali ya ufadhili na kuhakikisha ushiriki wa moja kwa moja na uwakilishi wa jamii za wanawake kutoka mikoa mbalimbali katika maeneo haya. Kwa mfano; Wanun Permpibul, mfuatiliaji wa jinsia wa kikanda wa GCF nchini Asia, kutoka **Climate Watch Thailand** (waangalizi wa hali ya anga Thailand), alishiriki katika mkutano wa bodi ya GCF na alichanguliwa kuwa katika timu ya waangalizi halisi ya makundi ya kijamii (CSOs). Wakati huo huo, utetezi wa pamoja wa makundi makubwa ya kijamii (CSOs), pamoja na GAGGA, ulisababisha kufutwa Kwa muda Kwa shirika la Benki ya Sumitomo Mitsui (SMBC)- mkopeshaji wa tatu duniani kwa watengezaji wa m ipango ya makaa ya mawe-kutoka kwa ajenda ya GCF ili SMBC kuboresha matumizi na sera ya uwekezaji wa nishati, ambayo haiambatani na malengo ya GCF na Mkataba wa Paris.

## Kutengeneza kesi kwa ufadhili bora

Pamoja na washirika wa kimikakati, Global Green Grant Fund (GGF) na Prospera- (mtandao wa kimataifa wa hazina ya wanawake), GAGGA ilifanya kazi ili kuimarisha maslahi na **kasi miongoni mwa wafadhili wa serikali na jumuiya ya uhisani** kwa kujumuisha, kubadilika, kutetea haki za wanawake, na kupelekeshwa na jamii. Ufadhili kwa ajili ya harakati za wanawake wa ndani ambazo zinaongoza hatua za kutetea mazingira na hali ya anga/hewa. GAGGA ilialikwa kwenda kupeana na kuonyesha kazi na matokeo yetu kwa Global Affairs Canada, ikijumuisha idara zake za fedha za hali ya anga na mifumo ya chakula na mazingira, na kukutanana United Kingdom Foreign Commonwealth and Development Office (ofisi ya jumuiya ya madola ya kigeni na Maendeleo ya Uengereza).

Global Green Grants Fund and prospera (Mtandao wa kimataifa wa hazina ya wanawake), waliendelea na kazi yao na **Funder Learning Community for Women and the Environment** (jumuiya ya wafadhili kujifunza kwa wanawake na mazingira, FLC), kikundi cha taasis za kibinafsi. Tathmini ya FLC ilionyesha kuwa asili mia themanini na mbili 82% ya waliohojiwa walikubali kwa dhati kwamba wamejifunza Jinsia wanawake wanavoongoza mipango muhimu ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya anga na uharibifu mwengine wa mazingira, na kwamba ujuzi wao ulibadilika/ na kuongeezeka 'kwa kiasi kikubwa' kwa wingi wa mada zilizojadiliwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Washirika na wanachama wa GAGGA walifanikiwa kushawishi wafadhili kutoa msaada kwa ajili ya kazi ya mazingira na hali ya hewa kwa wanawake, inayozingatia jinsia na hali ya hewa katika mwaka wa 2020.

- Mwaka wa 2020, **53% ya washirika wa GAGGA walionyesha kuwa walipokea ufadhili kutoka kwa wafadhili wapya** na kuongeza angalau hadi Euro millioni Moja nukta tisa (€1.9M)[1]. Hata hivyo, wakati wa ongezeko la wanafadhili wapya lilikuwa chanya, ni muhimu kutambua kwamba jumla ya kiasi cha fedha kilikuwa kidogo kuliko miaka iliyopita.

- **Wizara ya mambo ya nje ya Uholanzi ilichagua GAGGA kama mshirika wa kimkakati** chini ya mfumo wake wa sera ya mwaka wa elfu mbili ishirini na moja hadi elfu mbili ishirini na tano (2021-2025) Power of Voices (nguvu ya sauti). Mpango wa GAGGA wa 'Women Leading Climate Action' ulitunukiwa fedha Euro million thelathini na nne (€34M).

- Ford Foundation (Wakfu wa Ford), chini ya mfuko wake wa ufadhili mpya wa Resilient Women and Natural Resources Plus Fund, (Mfuko wa Fedha wa Wanawake Wastahmilivu na Rasilimi ilitoa ruzuku yake ya ufadhili kwa GAGGA Dola elfu mia moja ($100,000) ili kuongoza **uchoraji wa ramani ya vikundi vya wanawake vya kijamii, na mashirika** katika Global south (Kusini Kimataifa) yanayofanya kazi katika makutano ya haki za wanawake, mazingira na haki ya hewa. Uchoraji wa ramani unaangazia aina tofauti za **unyanyasaji wa kimuundo unao wakabili wanawake na wasichana watetezi wa mazingira au watetezi wa ardhi na maeneo yao** na namna wanavyoitikia.

[1] Hii haijumuishi ufadhili mpya ulipokelewa na wanachama wa muungano wa GAGGA, FCAM, Both ENDS na Mama Cash.

## Ushirikiano wa cross-movement na kejenga muungano

Katika muktadha wa janga la Covid-19, nguvu ya ushirikiano wa kipekee wa GAGGA wa harakati ulijidhihirisha kwa njia nyingi. Kwa haraka tulijifunza zaidi kuhusu hali halisi na mahitaji ya vuguvugu la ndani tulilounga mkono na kuona haja ya kurekebisha mipango ipasavyo. Mwezi Mei, GAGGA ilizindua **mfuko wa kujiendesha na kustahimili** (ARF), mpango wa wakati mmoja wa ufadhili uliolenga kushughulikia mahitaji ya dharura ya wanawake watetezi wa mazingira na jamii zao kupitia uimarishaji wa **mifumo inayoendeshwa na jamii ya ustahamilivu na uhuru** ambayo inategemea kanuni za usawa, mshikamano na utunzaji wa pamoja kwa watu na asili. Muundo wa mtandao wa GAGGA, hasa muhusiano na uaminifu unaowaezesha, ulionekana kuwa muhimu kwa mafanikio ya ARF katika muda wa wiki sita pekee (6 weeks), GAGGA ilipokea jumla ya maombi mia mbili na ishirini na moja 221, yakiwemo mia moja na tisini na tatu 193 kutoka kwa mashirika ya kijamii yaliyo na wanawake kumi na nane 18 kutoka kwa washirika wa NGO ya GAGGA. Katika kipindi cha miezi mitatu (3 months), GAGGA ilitoa **Euro elfu mia mbili na kumi na nne mia moja na nane (€214,108) kwa vikundi arubaini na moja (41) vya msingi na euro elfu arubaini mia mbili tisini na mbili (€40,292) kwa NGOs saba katika nchi ishirini na moja (21) duniani kote.**

Kufuatia hitimisho la mchakato wa utoaji ruzuki ya fedha, GAGGA iliagiza utafiti wa ARF ili kujifunza kuhusu na kuelewa uzoefu, mitazamo na mahitaji ya watetezi wa haki za mazingira za wanawake na jumuiya zao wakati wa shida. Ripoti hiyo, The Autonomy and Resilience Fund (mfuko wa fedha wa uhuru na ustahamilivu) katika kubadilisha hofu kuwa kutumaini, inachangia mijadala muhimu kuhusu ushirikishwaji, urahisi, utetezi wa haki za wanawake na rahisi mali zinazoendeshwa na jamii kwa ajili ya kazi ya haki ya jinsia, mazingira na hali ya anga, katika muda mfupi na pia muda mrefu.

## Sauti kutoka Kwa mtandao wa GAGGA

Kutoka tarehe nane hadi ishirini na mbili mwezi machi (8-22 march)- siku ya kimataifa hadi siku ya maji duniani- makundi ya mashiriki ya GAGGA katika America ya Kusini, yalifanya kampeni ya nne ya kila mwaka ya 'sisi wanawake ni maji' (We Women are water). Kampeni hiyo iliangazia jukumu na uongozi wa wawanawake wa Amerika Kusini Katika kutetea na kulinda maji, na kufichua madhara ambayo Wanawake wanateseka kutokana na unyonyaji na uchafuzi wa jambo hili la manufaa kwa wote. Kampeni wakati pale uzito wa janga la Covid-19 ulipokuwa ukidhihirika, kwa ujumbe muhimu ulikuwa umuhimu wa kuhakikisha haki za binadamu ya kupata maji safi na salama katika kukabiliana na janga la COVID-19 ikijumuisha hatua rahisi kama kunawa mikono.

GAGGA pia ilikuza uhamashaji na kufanya uhalisia wa wanawake wa eneo hilo pamoja na jumuia zao kuonekana wazi katika muktadha wa janga la Covid-19. GAGGA ilikusanya recodi takriban sitini 60 kutoka kwa washirika barani Africa, Asia na America Kusini, ambao walieleza uzoefu wao katika miezi ya kwanza ya janga hilo, hadithi hizo za sauti (audio stories), zilizoshirikishwa zaidi kwenye mtandao wa Twitter, zilifikiwa zaidi ya 17,500 na kusababisha mawasiliano zaidi ya 600 ya watumiaji wa mtandao wa twitter na pia kutangazwa na habari za nje.

## Ushirikiano na wizara ya Mambo ya nje ya Uholanzi

Mambo muhimu ya ushirikiano wa GAGGA na Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi mwaka wa 2020 ni pamoja na kuratibu **jedwali la wanawake, ushirikishwaji na mazingira,** ambalo liliwaleta pamoja wawakilishi arobaini 40 kutoka Canadian, Uholanzi, Ujerumani, Uswizi na Serikali za Uingereza zinazo shughulikia utungaji sera za mazingira na hali ya hewa, na kutoka taasisi za kibinafsi za Marekani na Ulaya.

Jedwali hilo liliandaliwa na Idara ya Ukuaji wa Kijani Shirikishi ya wizara na kuwezesha kubadilishana na kujifunza, kwa kuzingatia matokeo muhimu ya uchoraji wa ramani yetu, iliyofanywa mwaka 2019, kuhusu sera, taratibu, zana na njia za ufadhili zinazofaa za wafadhili watano wa serikali. GAGGA pia ilitetea **kuhakikisha kuwa ufadhili wa wizara wa janga la Covid-19 unawafikia wenyeji na jamii,** hususan wale kutoka kwa vikundi viivyokataliwa- wanawake, wenyeji asili, wakulima wa vijijini na pwani, na jamii za wavuvi- kupitia njia za ufadhili zilizoko.

## Mafunzo ya miaka mitano ya GAGGA

Kutokea mwaka 2016, GAGGA imetoa **Euro milioni kumi nukta mbili nne (€10.24M) katika ruzuku ya fedha elfu moja mia tano na kumi na nane (1518) kwa vikundi vya chini vinavyoshughulikia haki za wanawake na haki ya mazingira,** haswa kupitia hazina za haki za wanawake na mazingira. Tathminii ya mwisho ya nje ya program yetu ya kwanza ya miaka mitano ilihitimisha kuwa tumepata maendeleo makubwa katika kufikia malengo yetu ya miaka mitano.

Uzoefu wetu katika miaka iliyopita umeweka wazi umuhimu wa **kuleta pamoja haki za wanawake, harakati za haki za mazingira na hali ya hewa na kuzingatia ujuzi na uzoefu wa mashirika ya kijamii ya wanawake** katika hatua za mazingira na hali ya hewa, na pia katika sera za mazingira na hali ya hewa.

Wanawake, katika utofauti wao wote, wanachukua masuluhisho ya kijasiri, ya kiubunifu na ya jumla, sio tu kushughulikia uharibifu wa mazingira na athari mbaya za hali ya hewa wanazo kabiliana nazo sasa na siku zijazo, lakini pia kubadilisha ukweli wao na wa jamii zao. Tunapofunga miaka hii mitao ya kwanza, GAGGA, tunaweza kujivunia kile ambacho tumefanikiwa pamoja na kutarajia kuona mtandao ukikua na kupanuka.

fcam Fondo Centroamericano de Mujeres   mama cash   Both ENDS Connecting people for change